


# ITAFUTE ANWANI YAKO

"Ishi Kutimiza Kusudi Lako"

AVITH AMOS KANDUBUKA

Toleo la kwanza kwa lugha ya Kiswahili
Hatimiliki ©2022

Avith Amos Kandubuka
P.O.Box 1600, Bukoba
+255 753 161 261
avistar30@gmail.com


Sanifu jalada na:
RUSHMEDIA TANZANIA
P.O.Box  24887, Dar Es Salaam, Tanzania
+255 716 666 639 / +255 752 635 132
rushmediatanzania@gmail.com

Kufasiri na sanifu ya ndani ya kitabu:
DL Bookstore
+255 787 163 013
authors@dlbookstore.com
www.dlbookstore.com
Arusha, Tanzania

ISBN: 978-998-7030-93-4

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kunakiri, kutafsiri, kupiga chapa au kutumia aina yoyote ya elektroniki. Kwa kutoa upya nakala ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi.


# SHUKRANI



SHUKRANI.................................................................... v
WAZO.......................................................................... ix
UTANGULIZI.................................................................. xi
SURA YA KWANZA........................................................ 1
UMETUMWA KWA AJILI YA JAMBO FLANI............ 1
SURA YA PILI.................................................................. 9
HITAJI LA MOYO........................................................ 9
SURA YA TATU.............................................................. 19
UFUPI WA MUDA......................................................... 19
SURA YA NNE................................................................ 37
JAMBO MOJA................................................................ 37

SURA YA TANO........................................................ 43
NGUVU YA USUGU........................................................ 43
SURA YA SITA........................................................ 53
JADILIANA VYEMA NA BAADAYE YAKO................ 53
SURA YA SABA........................................................ 67
MAAJABU YA MANENO YAKO................................ 67
SURA YA NANE........................................................ 77
SHUGHULIKA NA AKILI........................................ 77
SURA YA TISA........................................................ 89
NDOTO ILIYOTELEKEZWA.................................... 89
SURA YA KUMI........................................................ 101
MFUMO WA ELIMU................................................ 101
SURA YA KUMI NA MOJA........................................ 119
KUSUDI LAKO LINAPOKUWINDA.......................... 119
SURA YA KUMI NA MBILI........................................ 127
ONDOKA KWENYE UKANDA WAKO WA RAHA... 127
SURA YA KUMI NA TATU........................................ 141
MTI USIOZAA MATUNDA........................................ 141
SURA YA KUMI NA NNE........................................ 153
BETRI YA MAISHA................................................ 153

# SHUKRANI



Kwanza kabisa, sifa na shukurani ni kwa Mwenyezi Mungu kwa baraka na rehema zake zisizo na kikomo, maarifa na nguvu. Kuandika kitabu hiki si kazi rahisi lakini kwa uwepo wa Mungu kila kitu kimewezekana kwangu.

Ningependa kutoa shukurani zangu za kipekee kwa watu ambao wamekuwa walimu kwangu kwa kufahamu ama pasipo kufahamu lakini kwa kupitia karama walizojaaliwa na Mungu wamenifanya mimi kuwa hivi nilivyo leo, nikianza na Dkt. Renald Rweyemamu, Mwl. Christopher Mwakasege, Mch. Dkt. Eliona Kimaro, Mch. Carlos Kilimbai, Askofu TD Jakes, Dkt. David Oyedepo na Mwl. Sir Bill Mush.

Ninatoa shukurani pia kwa wazazi wangu, ahsanteni sana kwa upendo wenu, sala zenu, kujali kwenu na jitihada pasipo kuchoka katika kunitia moyo kufanya zaidi na zaidi.

Kuwa na marafiki wazuri ambao daima wanaamini katika unachokifanya na wanaotamani kukuona ukifanikiwa ni baraka tele kwenye maisha. Deus Vicent, Arch. David Joseph na Magdalena Murasa ahsanteni kwa jitihada zenu bila ya kuchoka, kunisukuma na kunitia moyo kuandika na kukimaliza kitabu hiki..

Ninatoa shukurani za dhati kwa rafiki na kaka yangu mkubwa, Innocent Anicet kwa muda wako, nguvu na rasilimali ulivyowekeza kuhariri kitabu hiki. Mungu abariki kipaji chako na kufanikisha katika kazi zako.

Kwa dada yangu Reatha Byera Shwekerela, wewe ni baraka maishani mwangu. Ninamshukuru Mungu kwa kukujalia moyo wa hisani usioshindwa. Ubarikiwe kwa juhudi na muda uliojitolea kuhariri kitabu hiki hadi hatua ya mwisho.

Kwa ndugu Dickson Kirenga, ubunifu na fikra zako vimekuwa zaidi ya matarajio yangu, ahsante sana.


Shukrani kwa DL BOOKSTORE kwa kufasiri kitabu hiki kutoka lugha ya Kiingereza na kisha kufanya sanifu kurasa yake (ubunifu wa ndani ya kitabu).

Pia, shukrani za pekee kwa RUSHMEDIA TANZANIA kwa kufanya sanifu jalada ya kitabu hiki. Nyote kwa pamoja, Mungu aibariki kazi yenu na kuwapa mafanikio katika kila kazi muifanyayo.

*Kutabaruku*

*Kwa kila Kijana ulimwenguni na kwa yeyote mwenye ndoto ya kuacha alama kabla hajaondoka humu duniani. Fursa na nafasi ya kufanya miujiza mikubwa bado ipo, ni wakati wako sasa.*

# WAZO




Wazo la kitabu hiki lilianzia kanisani, wakati Mch. Dkt. Eliona Kimaro wa KKKT Usharika wa Kijitonyama (Kush Turbanacle) kupitia ibada ya masifa ya jioni alipohubiri kuhusu kujitafuta na mwishowe kutoa zoezi la kila mmoja kwenda na KUITAFUTA ANWANI YAKE ili kuleta matokeo kwenye chochote akifanyacho.

Tangu wakati huo, nimekuwa nikiisikia sauti ya Roho Mtakatifu ikininong'oneza moyoni mwangu kuwa *'TAFUTA ANWANI YAKO'*. Kwa nyakati tofauti nimekuwa nikikiona kitabu kwenye maoni yangu kikiwa kimeandikwa Tafuta Anwani Yako na wakati huo nilikuwa nikiandika kitabu kingine kiitwacho *"There is Still a Chance"*. Niliiahidi nafsi yangu ningeandika kitabu kiitwacho Tafuta Anwani Yako mara tu nitakapokimaliza kitabu nilichokuwa nikikiandika, na leo ninafurahi kuitimiza ahadi yangu. Ninatumaini kitabu hiki kitakusaidia kujitafuta.

*“Naye alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani, na mipaka ya makazi yao.”*

*MATENDO 17:26*

# UTANGULIZI



Nikiwa mwaka wa mwisho wa shahada yangu ya kwanza, nilikuwa na wazo kichwani mwangu kuomba nafasi ya mafunzo kwa vitendo kwenye Shirika la Viwango la Taifa (Tanzania Bureau Standards - TBS). Nilikuwa na shauku ya kufahamu namna viwango vinavyoandaliwa na mchakato wote wa kuvijaribu kwa kutumia vifaa vya kitaalamu na vitu vingine vihusianavyo katika idara ya Uhandisi Mitambo. Niliandika barua na kuituma kwa mmoja wa Rafiki yangu aliyekuwa Dar es Salaam ili anisaidie kuifikisha barua hiyo makao makuu ya shirika hilo Ubungo. Niliamini, endapo barua yangu ingefikishwa kwa mkono ingekuwa rahisi kuzingatiwa kuliko ningetuma kwa njia ya posta.

Rafiki yangu Jack aliipokea barua hiyo iliyoambatanishwa na wasifu wangu, akaichapa na kuifunga bema katika bahasha na juu ya bahasha akaandika anwani. Kutokana na mambo yasiyotarajiwa hakupata wasaa wa kuifikisha barua ile moja kwa moja kwenye ofisi

za TBS, hivyo kaamua kuituma kwa EMS. Aliamini mfumo huo ungekuwa rahisi kuliko kwenda yeye ofisini. Si punde alinipa mrejesho wa kile alichokifanya na nilimshukuru kwa sababu alinisaidia licha ya kutokuwa katika namna niliyoipanga awali.

Baada ya siku mbili nilipokea simu kutoka TANESCO, sauti nyororo ikiniambia, *"Tumepokea barua yako iliyoandikwa Tanzania Bureau of Standards (TBS) lakini ina anwani ya TANESCO"*. Nikaeleza kilichotokea ni makosa ya uandishi wa anwani ya mahali barua ilipopaswa kwenda. Nilipomalizana na TANESCO nilishangazwa sana ilikuwaje Jack aliandika jina sahihi la shirika lakini akakosea kuandika anwani. Ingawa jina liliandikwa sahihi anwani ilikosewa na hata kufanya barua kwenda mahali isipokusudiwa.

Tunakuja duniani tukiwa na anwani mahususi na za kipekee. Unapaswa kukumbuka kuwa jina lako siyo anwani yako kwa sababu majina hutumiwa na watu tofauti, unacho kitu kingine zaidi ya jina lako. Kitu kinachokutambulisha wewe na kukufanya kuwa wa tofauti na kitu hicho ndiyo anwani yako. Hakuna mtu anayeshiriki anwani yake na mtu mwingine. Anwani hii ndicho kitu kinachokufanya wewe kuwa wa kipekee na uweze kufanya vitu ambavyo watu wengine hawawezi kuvifanya. Tunafanana majina, tarehe za kuzaliwa lakini tuna anwani tofauti za maisha, tunaweza kuwa mapacha tunaofanana lakini tutatofautiana anwani zetu. Kuitafuta anwani yako ni kujitafuta, kujitambua vile hasa ulivyo. Kujitambua kutakuweka mahali sahihi na kuletea matokeo makubwa duniani. Ukijifahamu wewe ni nani, moja kwa moja utafahamu wewe si nani.

Kushindwa kuitambua anwani yako kutakuweka mahali kusiko sahihi na utaishi maisha yenye madhila mengi na kupelekea

matatizo duniani. Kama tu ilivyokuwa barua ya kwenda TBS lakini pasipo kutegemea ikaenda TANESCO, barua haikuwa na matokeo yoyote kule TANESCO zaidi ya kusababaisha tu usumbufu kule na kujaza uchafu wa makaratasi. Lakini endapo anwani ingekuwa sahihi, barua ile ingekuwa imefika mahali sahihi na kuleta matokeo yaliyotarajiwa tangu mwanzo, kwamba ningepata nafasi ya mafunzo kwa vitendo. Sikupata nafasi hiyo kwa sababu barua ilikwenda mahali kusiko sahihi.

Hivi ndivyo wengi wetu tunavyoishi na maisha yetu yote kuwa na taaluma zisizo sahihi, kazi zisizo sahihi, ndoa zisizo sahihi na vitu vingine vingine vinavyotupeleka mahali kusiko sahihi. Mazingira tunayoyaishi yana msukumo mkubwa katika kubadili anwani zetu ndiyo maana pale unapofahamu umuhimu wa kuitafuta anwania yako ya pekee itakupa sababu ya kupingana na kile ambacho asili inajaribu kukwambia. Kama tu ilivyo kwa simba aliyepata kuishi kama kondoo, simulizi niliyopata kuisoma kwenye moja ya vitabu vya Dkt. Myles kinachoitwa "ROHO YA UONGOZI"

> *"Hapo kale paliondokea mkulima aliyeishi kwenye kijiji flani huku pia akifuga kondoo. Siku moja, alimpeleka kondoo wake malishoni, na alipokuwa akichunga, ghafla alisikia sauti ya ajabu ikitokea kichakani, ambayo awali ilisikika kama ndama. Akiongozwa na udadisi wake, mchunga kondoo alikwenda kutazama chanzo cha sauti hiyo na alishangazwa kumwona mtoto wa simba akitaabika kutokana na kupotezana na familia yake.*
>
> *Wazo lake la kwanza lilikuwa angeingia matatizoni endapo angeendelea kumsogelea yule mtoto wa simba na wazazi wake wakarejea. Hivyo, mchungaji huyo alifanya haraka kuondoka eneo hilo na kuendelea kutazama kutoka mbali ili kuona kama mama wa mtoto wa simba angerejea. Hata hivyo, baada ya jua kuanza*

*kuzama, na hakuna kilichokuwa kikiendelea kumnusuru mtoto wa simba, mchungaji akaamuwa, kwa ajili ya usalama wa yule mtoto wa simba, kumchukua hadi nyumbani kwake ili kumtunza.*

*Kwa zaidi ya miezi minane, mchungaji alimlisha mtoto wa simba kwa mikono yake, kumpa maziwa na kumtunza mahali salama na penye joto ndani ya nyumba yake. Mtoto wa simba alipokuwa kiasi cha kuanza kucheza na kuwa thabiti aliambatana naye kila siku kwenda kuchunga kondoo. Mtoto wa simba alikuwa sambamba na kondoo na kuwa sehemu ya uchungaji kondoo. Kondoo wakamkubali na kumwona miongoni mwao. Baada ya miezi kumi na mitano kupita, simba mtoto alikuwa tayari mkubwa lakini alienenda, kutenda na kutoa sauti kama kondoo. Kiasi kwamba simba alikuwa sasa ni kondoo kutokana na mchangamano wao. Alijipoteza na kuwa kondoo. (Kwa kifupi alipoteza anwani yake halisi kwa sababu ya namna alivyolelewa)*

*Siku moja mchana, mchunga kondoo aliketi juu ya mwamba, akijipumzisha kivulini. Aliitazama mifugo yake ikinywa maji yaliyokuwa yakitiririka. Simba, aliyejidhania kuwa kondoo aliwafuata kunywa maji. Ghafla, ng'ambo tu ya mto lilitokea kundi kubwa la simba ambalo yule simba mtoto hakupata kuliona kabla. Kondoo walichanganyikiwa, na wakiongozwa na hisia za kutaka kujiokoa, walitoka kwenye maji na kukimbilia uelekeo wa shamba. Hawakusimama hadi walipokuwa ndani ya uzio. Jambo la kushangaza, hata yule simba ambaye alishakuwa mkubwa alikimbia nao, akizongwa na hofu.*

*Wakati kundi la kondoo likipambania usalama wao, kundi la simba lilitoa sauti iliyolitetemesha pori lote. Alipokinyanyua kichwa chake juu ya nyasi ndefu, mchungaji alimwona kondoo*

*mmoja akiwa ametapakaa damu kuonesha yu mfu. Akatambua hatari iliyowaingia.*

*Takribani siku saba ziliyoyoma pasipo tukio jingine, na pale alipokuwa akiwachunga kondoo wake, yule simba mtoto alishuka kondeni kunywa maji. Alipoyainamia maji, alipatwa na mshituko wa ghafla na kukimbia kuelekea nyumbani. Kondoo hawakukimbia isipokuwa kumshangaa kwa nini alikimbia, huku yeye akiwashangaa kondoo kwa kutokimbia ilihali amemwona simba tena. Baada ya kitambo kifupi, simba mtoto alikwenda taratibu kuungana na kundi la kondoo na kushuka kondeni ili kunywa maji tena. Kwa mara nyingine tena alimwona simba na kuchanganyikiwa, jambo ambalo hakulijua, ilikuwa taswira iliyomuakisi yeye mwenyewe ndani ya maji.*

*Huku akiendelea kujaribu kuelewa kile alichokuwa akikiona, ghafla, simba alijitokeza tena kutoka msituni.*

*Kundi la kondoo lilikimbia kwa kasi kubwa kuelekea nyumbani, lakini kabla simba mtoto hajavuta hatua yake, simba alivuka maji kumwelekea huku akitoa sauti kali iliyomwumiza masikioni mwake huku ikilijaza pori zima. Kwa kitambo fulani, simba mtoto alihisi maisha yake yamefikia ukingoni. Akang'amua kwamba alichokiona si simba mmoja bali wawili, mmoja akiwa majini na mwingine mbele yake.*

*Kichwa kilimgonga kutokana na kuchanganyikiwa kadri simba alivyomkaribia na nyuso zao kukaribiana huku akionesha nguvu ya kutisha katika namna iliyomwambia, "Jaribu, njoo na unifuate."*

*Kadri hofu ilivyomvavagaa, simba mtoto aliamua kujaribu kuunguruma kama simba. Hata hivyo, sauti pekee aliyomudu*

*kuitoa huku akiumiza taya zake ni sauti ya kondoo. Simba alimjibu kwa sauti nzito zaidi kana kwamba anamwambia, "Jaribu tena." Baada ya kujaribu mara saba ama nane hivi, ghafla simba mtoto alijisikia akiunguruma kwa sauti yenye kufanana na ya simba mbele yake. Alijisi misuli kukaza, jambo ambalo hakupata kujisikia hapo kabla. Ilikuwa kama mwenye kupata mabadiliko makubwa katika akili, mwili na roho.*


*Ghafla, mtoni pale walisimama simba wawili wakitazamana. Mchungaji kondoo alikiona kitu ambacho hatokisahau kamwe. Kadri miungurumo ya simba ilivyolijaza pori, simba mkubwa alinyamaza, akageuka na kumpa mgongo simba mtoto na kuanza kutembea kuelekea porini. Kisha, alisimama na kumtazama simba mtoto na kutoa sauti kana kwamba anamwuliza, "Unakuja?"*

*Simba mtoto alielewa maana yake na papo hapo akatambua siku yake ya kufanya maamuzi imewadia ili achague endapo aendelee kuishi kama kondoo ama kuwa ile nafsi aliyojitambua nayo. Alifahamu kwamba kuwa yeye halisi, alipaswa kuachana na maisha salama, yanayotaburika na rahisi kule nyumbani kwa mchungaji na badala yake kuingia kwenye maisha magumu yenye kuogofya, yasiyotabirika na ya hatari nyingi msituni. Ilikuwa siku ya yeye kuwa nafsi ya kweli na kuacha ile taswila ya maisha mengine nyuma yake. Ulikuwa mwaliko wa "kondoo kuwa mfalme wa pori." Muhimu zaidi, ulikuwa mwaliko kwa mwili wa simba kumilikiwa na roho ya simba.*

*Baada ya kutazama mara kadhaa mahali lilipo shamba la mchungaji na pia mahali lilipo pori, simba mtoto aliwapa mgongo shamba na kondoo alioshi nao kwa miaka, na kumfuata simba kuelekea pori ili kuwa vile alivyoumbwa kuwa daima, mfalme simba.*

Tafuta Anwani Yako ni kitabu kilichoandaliwa kukuamsha akilini mwako ili uhamasishwe na kuanza kukifanya kile kinachotakiwa ili kuipata anwani yako halisi, kutafuta mahali unapotakiwa kuwa na nini unachoweza kukifanya na kukizingatia hadi pale jambo fulani litakapozaliwa kwayo. Kutengeneza dhamira ya dhati ya kujitambua na kutumia fursa zako ni jambo la sasa na si la baadaye, kuwa wewe ni jambo unalopaswa kulifanya katika maisha yako yaliyobakia. Mtu mmoja mwerevu alipata kusema, *kuna siku mbili muhimu kwa kila binadamu humu ulimwenguni; siku aliyozaliwa na siku anayolitambua kusudio la kuzaliwa kwake.* Kisome kitabu hadi mwisho na utafurahia yaliyomo.

# SURA YA KWANZA



## UMETUMWA KWA AJILI YA JAMBO FLANI

*"Ulikuja duniani humu kwa kuwa kuna kitu dunia ilikihitaji na Mungu alikificha kitu hicho kwako." - Dkt. Myles Munroe*

Kuna mapengo mengi duniani yanayopaswa kuzibwa na watu kwa kutumia vipaji vyao, talanta na upekee ili kuifanya dunia kuwa bora zaidi kwa ajili ya binadamu na viumbe vingine vyote. Pasipo kuifahamu anwani yako halisi (nafasi yako) utakwenda tu mahali popote na kufanya kila kitu lakini utashindwa kuliziba pengo unalopaswa kuliziba, na mwishowe utasababisha tu matatizo badala ya kuyatatua. Nikitazama jambo hili ninakumbushwa moja ya filamu ninazozipenda iitwayo **Ghost in the Dark** *(Mzimu Kizani).* Filamu hii inatokana na kisa cha kweli panapo mwaka 1896 wakati wa ukoloni pale ambapo Waingereza waliamua kujenga

reli kwenye makoloni yao ya Afrika Mashariki, ikianzia bandari ya Mombasa nchini Kenya ya sasa na kuelekea Ziwa Viktoria na hatimaye Uganda.

*Wakoloni wa Kiingereza walitumai kuwa reli ingewahamasisha watu kuhamia maeneo ya ndani ya Afrika na kwamba ingetoa nyenzo ya usafirishaji bidhaa baina ya Afrika na Ulaya. Maelfu ya vibarua waliletwa kutoka India ili kuijenga reli ambayo ilikusudiwa kuwa na urefu wa maili 580 ikivuka mitoa na mabonde kadhaa na kuchukua miaka 30 ili kukamilika huku ikifika Nairobi mwaka 1899, na Kisumu pembezoni mwa Ziwa Viktoria mwaka 1901 na kufika Kampala, Uganda mwaka 1928. Ilitazamwa kama ishara ing'aayo ya maendeleo ya Waingereza katika kulistaarabisha bara ambalo lilifahamika kama 'Bara la Giza'.*

*Mwezi Februari 1898, ikiwa ni miaka miwili tu tangu ujenzi uanze, reli ilifika Mto Tsavo nchini Kenya, ikiwa ni maili 130 kaskazini mashariki ya Mombasa. Daraja la muda mfupi lilijengwa ili kuruhusu vifaa kuvushwa na ujenzi kuendelea upande wa pili. Mwezi Machi, Kanali wa Jeshi la Uingereza, John Henry Patterson aliletwa kutoka India ili kusimamia ujenzi wa daraja la kudumu la reli juu ya mto huo. Bonde la mto lilikuwa na upana wa yadi 100. Patterson alianza kwa kutafuta vyanzo vya mawe takribani maili tatu mbali na hapo na kujenga reli ndogo kwa ajili ya kuyasogeza hadi eneo la ujenzi. Mawe hayo yalikusudiwa kutumika kwa ajili ya kujengea msingi kwenye kina cha mto na baadaye kujenga nguzo za daraja. Wakati huo huo, ujenzi wa reli kuu uliendelea. Kwa sababu ya haya, maelfu ya wafanyakazi walitawanyika huku na kule kwenye makambo mbalimbali pembezoni mwa reli umbali wa maili 20. Patterson ndiye aliyewajibika juu yao wote.*

*Ikiwa ni siku chache tu tangu kuwasili kwa Patterson, watu walianza kutoweka.*

*Mwanzoni, Patterson hakuwaamini wenyeji waliomwambia kuna simba waliokuwa wakiwavamia wafanyakazi. Si punde, hata hivyo, taarifa za kuonekana kwa simba zilianza kumiminika, na mabaki ya wafanyakazi kupatikana. Ikabainika uwepo wa simba wawili hivi waliohusika. Siku chache baadaye, simba mmoja alivamia miongoni mwa kambi zilizotawanyika, kisha nyingine akiwavamia farasi, punda, mbuzi, ng'ombe na watu. Wafanyakazi wa Kihindi wakajenga uzio kuzunguka kambi zao zikijulikana kama boma, ambazo zilitengenezwa kwa matawi ya miiba ya miti ya mipogoro, na kukoka moto uliowaka usiku kucha, lakini bado simba walipata njia za kuingia. Katika tukio moja, mmoja wa simba alitambaa hadi kwenye hema na kumvamia mfanyakazi aliyekuwa usingizini, lakini akiwa katika mshituko, simba alilivuta godoro badala ya mfanyakazi huyo – na alipoling'amua kosa lake, simba alilitupa godoro na kukimbia.*

Kuifupisha simulizi hii, hili tatizo la wafanyakazi, ng'ombe, mbuzi na kondoo kuwindwa na kuuawa na simba liliendelea kwa siku kadhaa na ujenzi wa reli ukawa mgumu zaidi kuendelea kutokana na morali ndogo ya wafanyakazi waliobakia. Kanali John Henry Patterson akapata changamoto kubwa ya kufanikisha kazi aliyoaminiwa na serikali ya Uingereza.

Hakutaka kukata tamaa na hivyo akaamua kutumaini mikakati tofauti ya namna ya kuwashinda simba. Alitengeneza mikakati iliyoshindwa moja baada ya mingine na matukio ya simba kuwavamia yaliongezeka kadri siku zilivyokwenda kiasi cha baadhi ya wafanyakazi kuvunjika mioyo na kuamua kuacha kazi na kurejea makwao. Kutokana na ujasiri na uthubutu wa Patterson katika

kuwawinda simba, alikesha usiku kucha ndani ya mkokoteni ili kumwinda simba atakayeingia. Roho yake ya kutoshindwa kwa kujaribu mbinu tofauti ilileta matokeo chanya baada ya kufanikiwa kuwaua simba wote waliokuwa wakiwavamia.

Simulizi hii ya John Henry Patterson inafanana na kila mmoja wetu ulimwenguni; tumeletwa humu duniani, kwa kuaminiwa na Mungu wetu wa mbinguni (muumbaji wetu) ili tuje duniani kutatua matatizo yaliyo katika maeneo tunayoishi. Matatizo haya ni mengi kuanzia magonjwa sugu, Umasikini, ukosefu wa ajira, vita, ugaidi, uchafuzi, mabadiliko ya hali ya hewa ama kuongezeka kwa joto la dunia na mengine mengi unayoyaona. Hii ni ishara kuwa kuna watu mahali fulani ulimwenguni wenye suluhu ya haya matatizo. Sababu ya wewe kuendelea kuyaona matatizo haya ni kwa kuwa wengi wetu hatutimizi wajibu wetu kutumia fursa zetu kuyatatua. Kila mara huwepo visingizio vya sisi kutotumia karama zilizojificha ili kuinufaisha jamii tuishiyo.

Tumia muda mfupi, fikiria, nini kingetokea endapo kila mmoja angekuwa kama wewe, kutoa visingizio kadha wa kadha ili asitoe majibu ya mambo makubwa ulimwenguni, dunia ingekuwaje? Pengine, dunia hii ingekuwa mahali pabaya zaidi kuishi. Lakini, wewe nami tunafurahi uzuri wa kila kitu kinachotuzunguka kwa sababu tu kuna watu waliothubutu kufikiria na kuja na kile ambacho jamii inakihitaji. Dunia ina njaa na kamwe haitoshiba. Kila wakati dunia inahitaji mawazo mapya kufanyiwa kazi, ndoto mpya kutimizwa. Bado kungali na mapengo yanayohitaji kujazwa na uwezo na ujuzi tuliojaaliwa na Mungu. Tafuta mahali unapofaa, hiyo ni anwani yako, hiyo ni nafasi yako. Kama utaigundua anwani yako basi dunia itaandika simulizi yako na vizazi na vizazi vitaisoma simulizi yako na utakumbukwa.

Wengi wetu tumetingwa kufanyia kazi ama kupambania mambo mengi maishani, lakini hatutumii muda wetu kufikiria kwa nini tupo hapa na tungali hai hadi sasa. Siyo bahati tu kwamba ungali na pumzi leo, ni kwa sababu lipo jambo ambalo ni lazima ulifanyie kazi na kuleta matokeo duniani. Lipo duhumi unalopaswa kulifanyia kazi kabla muda haujakutupa mkono.

Tazama kile ambacho Biblia inasema juu ya Mfalme Daudi, *"Kwa maana Daudi, akiisha kulitumikia shauri la Mungu katika kizazi chake, alilala, akawekwa pamoja na baba zake, akaona uharibifu." (Matendo 13:36)* Daudi alikuwa mfalme, alikuwa mwanasiasa kama tungezungumza kwa lugha ya leo. Hakuwa mhubiri wala padri, lakini alikuwa kiongozi wa watu katika dunia ya kisiasa lakini alitumikia kusudi la Mungu. Hii inamaanisha unaweza kusimama na kutumikia kusudi la Mungu katika nafasi yoyote katika kizazi chako, kitu cha pekee unachopaswa kukifanya ni kutambua wapi ambapo Mungu anataka uwe.

John Henry Patterson Kanali wa Jeshi la Uingereza alitumwa kutoka India kusimamia ujenzi wa daraja la kudumu la reli akielewa fika alichokuwa akikitafuta barani Afrika. Alibakia kwenye anwani yake licha ya changamoto kubwa alizokumbana nazo, alisimama imara hadi mwisho. Afrika palikuwa eneo zuri palipomvutia kila mtu kutoka Ulaya na Mashariki ya Mbali kuja na kuwekeza katika kilimo na fursa zinginezo za kibiashara zilizokuwepo wakati huo. Kanali huyu wa Jeshi la Uingereza hakuondoka kwenye dhamira yake ya kufanyia kazi fursa zilizokuwepo, kama ambavyo wengi wangefanya leo. Aliendelea kuwa thabiti na kujipa muda kukamilisha dhamira yake moja, nayo ni kwamba, daraja lazima lijengwe.

Hakulala usiku wala mchana akiitafuta namna ya kuwashinda simba ambao waliendelea kuwavamia. John angeweza kukata tamaa ya dhamira yake ya kuanza biashara ya vipusa ambayo ilikuwa na faida kubwa nyakati hizo, lakini hakufanya hivyo. Kuufahamu wito wako na kuufanyia kazi ndicho ninachokiita kuitafuta anwani yako, ni jambo kubwa kufahamu wewe ni nani na kufahamu unafaa kuwa wapi. Kama ni kukukumbusha leo, wacha nikukumbushe kuwa sasa hivi unapaswa kuyafanya maisha yako ya thamani kwa kutafuta anwani yako. Acha kuishi ilimradi, maisha hayatakulazimisha kutafuta anwani yako lakini utapaswa kutengeneza matakwa ya ndani ili kukusukuma kujitafuta.

## Anwani ya Yohana Mbatizaji

Ukisoma kitabu cha Yohana, utakutana na mtu huyu aitwaye Yohana Mbatizaji, ambaye alipoulizwa yeye ni nani, alisema, *"mimi ni sauti niliaye nyikani nikiandaa njia kwa ujio wa Bwana"*. Yohana lilikuwa jina lake, lakini hakujitambulisha kama Yohana isipokuwa alijitambulisha kwa kurejea kusudi maalumu alililoletwa kulitimiza. Yohana alitumwa kusafisha njia kwa ajili ya ujio wa Yesu. Anwani yake ilikuwa kusudio lake, alikusudiwa kutengeneza njia kwa ajili ya Yesu na ujumbe wake mkuu ulikuwa, *"Tubuni, ufalme wa mbingu u karibu"*. Walimwita Mbatizaji kwa sababu aliwabatiza wale wote walioupokea ujumbe na kutubu dhambi zao. Maisha ya Yohana yaliakisi ujumbe wake, akiishi nyikani akila nzige na asali.

Wakati uliotolewa unabii juu ya ujio wa Mesia ulikuwa ukingoni, lakini kulikuwa na uhitaji wa kumtuma mtu ili kuandaa njia kwa ajili ya ujio wa Mesia. Muumba alimuumba mtu aitwaye Yohana aliyekuwa na sifa za mtengeza njia, kuandaa ujio wa Yesu. Jaribu kufikiria kwa kina jambo hili, fikiria kama Yohana angetingwa na mambo ya ulimwengu kiasi cha kusahau kusudi lake. Jambo hili

lingeleta madhara kuliko mema kwa sababu lingepeleka kuchelewa kukamilika kwa ujio wa Yesu. Anwani ya Yohana ilikuwa Sauti iliayo nyikani na siyo mijini, fikiria ungekuwa na jukumu la kumtafuta Yohana ungekutana na watu wengi waitwao Yohana, lakini endapo ungemtafuta Yohana Mbatizaji ungelazimika kusema kwa Uhakika juu ya anwani yake na ungempata pasipo shaka. Sauti ya Yohana ililia nyikani na siyo mjini lakini isivyo bahati alifika mjini na kuyaona maovu aliyoyatenda Herode na Yohana aliyalaani kiasi cha kumfanya Herode amtupe gerezani na mkewe akipiga kelele Yohana auawe.

Simulizi hii ya Yohana inatufundisha kuzifahamu anwani zetu halisi za maisha, mahali tunapotoshea. Si kweli kuwa tunatosha kila mahali, lakini tuna nafasi mahususi tunazopaswa kuzizingatia na kutumia vipaji vyote tulivyopewa na Mungu. Kuna watu walianza makusudi yao vema, wakaanza kupiga hatua za mafanikio lakini kwa sababu hawakuifahamu mipaka ya makusudi yao wakajikuta mahali ambako maisha yaliwageukia.

Umeagizwa kufanya kitu na siyo kuishi ilimradi tu, tafuta na uwe hivyo. Kama Mungu anataka kukutana nawe leo, atakupata wapi? Ndiyo, inawezekana Mungu akakubariki ukiwa mahali popote lakini zipo baraka zako zilizoelekezwa mahali pako na huwezi kuzikuta kwingineko zaidi ya kwenye anwani yako mahususi. Nafasi yako i wapi duniani?

Nafasi yako wala siyo ile nyumba uliyoijenga karibu na mji, ama lile jengo ulilopanga, lakini ni kile ukifanyacho katika kuhakikisha unachangia kuifanya dunia hii kuwa mahali bora zaidi. Umeagizwa jambo fulani humu duniani, acha kupoteza maisha yako kwa kuishi ilimradi tu. Ujumbe wa Yohana kwa kizazi chake ulikuwa *Tubuni, ufalme wa mbingu u karibu.*

Sasa, ujumbe wako ni nini kwa ulimwengu, Rafiki mpendwa? Maisha yako hutoa ujumbe duniani, ukifanyacho kila siku ni ujumbe ulimwenguni. Kama unatumia muda wako mwingi kwa mambo yasiyo na maana, basi unajaribu kuiambia dunia kuwa hujui kwa nini upo. Anza kuishi maisha yenye makusudi kwa kuanza kufanyia kazi kusudi lako kwa sababu muda hautoshi. Ninakwambia kwa hakika, katika kutafuta anwani yako ndiyo karama yako. Muumba amekukusudia kutawala dunia, lakini huwezi kutawala kila kitu duniani. Kuna nafasi mahususi ambayo ukiigundua na kuunganisha vipaji, ujuzi na uwezo wako kwenye nafasi hiyo mahususi, niamini kuwa wala hutomhitaji nabii kukwambia kuwa utaleta matokeo makubwa humu duniani. Asili yenyewe itajifunua kwa ajili yako na kukutambulisha ulimwenguni. Hutohangaika kuwafanya watu kukufahamu. Utakuwa maarufu moja kwa moja kwa sababu umekuwa vile Mungu alitaka uwe.